

## Maswali

1. Yakobo alikuwa na wana wangapi?
2. Mwana gani alipendwa na Yakobo?
3. Yakobo alipea Yusufu nini?
4. Yusufu aliota nini?
5. Yusufu alipendwa na nduguze?
6. Ndugu zake walimfanyaje Yusufu?
7. Walipokuwa wakila chakula nani walikuja?
8. Wafanya biashara walipofika ndugu zake Yusufu walimfanya nini?
9. Wafanya biashara walipeleka Yusufu wapi?
10. Nani alikuwa akilinda Yusufu alipokuwa nyumbani kwa Potifa?

## Majibu

1. 12
2. Yusufu
3. Koti la kipekee la rangi nyingi.
4. Miganda ya nafaka ya nduguze ziliinamia mganda wa Yusufu.
5. Hapana. Nduguze walimchukia.
6. Ndugu zake walimtupa kwa shimo.
7. Wafanya biashari walitokea.
8. Nduguze walimuza Yusufu kwa wafanya biashara kwa vipande 20 vya fedha.
9. Wafanya biashara walienda na Yusufu mpaka nchi ya Misri.
10. Mungu alimlinda Yusufu alipokuwa kwa nyumba ya Potifa.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1



## 11 Koti la Yusufu

**Kwa Biblia** Mwanzo 37

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba wivu na chuki huelekeza watu kufanya makosa.

### Somo

Yakobo aliishi Hebroni. Alikuwa na familia kubwa, watumishi wengi na kundi kubwa la kondoo. Yakobo aliishi kwa kambi kubwa ndani ya mahema. Yakobo alikuwa na wana kumi na wawili. Wana kumi wa kwanza walichunga kondoo. Mara nyingi walisafiri mwendo mrefu wakitafutia kondoo nyasi na maji. Hawa wana kumi walikuwa wabaya, hawakukuwa waaminifu na mara nyingi walisema uongo.

Wana wadogo wawili, mda mwingi walikaa nyumbani na familia kambini. Walikuwa wana wa Raheli, mkewe mpendwa wa Yakobo. Mwana wa Raheli mkubwa alikuwa Yusufu, na mdogo alikuwa Benyamini. Kwa ajili Raheli alikuwa amekufa, Yakobo aliwalinda hao zaidi.

Yakobo alifundisha Yusufu kumpenda Mungu. Alimfundishi kuwa mtiifu, mwaminifu na wa kutegemewa. Yakobo alimpenda Yusufu zaidi kuliko wana wengine. Yakobo alitengenezea Yusufu koti la kipekee. Lilikuwa koti la rangi nyingi. Ndugu zake wakubwa walipoona amevaa hilo koti la kipekee, walimwonea wivu.

Yusufu alikuwa na ndoto zizizo za kawaida. Aliota kwamba ndugu wote walikuwa shambani. Ilikuwa ni wakati wa kuvuna na walikuwa wakifunga miganda ya nafaka. Mganda wa Yusufu ulisimama katikati ya shamba. Miganda ya nduguze yote ikainama mbele ya mganda wa Yusufu. Yusufu aliambia nduguze juu ya hii ndoto. Walikasirika sana na kumwambia, "Hatutawahi kukuinamia." Ndugu zake Yusufu walimchukia kwa sababu ya koti na ndoto.

Siku moja ndugu zake Yusufu walienda Shekemu kutafutia kondoo nyasi. Baada ya mda mfupi Yakobo alituma Yusufu kwenda kuona vile ndugu zake walikuwa wakiendelea. Yusufu alisafiri mpaka Shekemu. Hakuwapata kule. Mtu moja akamwambia kwamba walikuwa Dothani. Kwa hivyo Yusufu alisafiri mpaka Dothani kutafuta Ndugu zake.

Ndugu zake walimwona akija na wakamchukia. Waliamua kumuua wakisema, "Mwotaji anakuja. Tutamua. Tutaambia baba yetu kwamba mnyama mkali alimua. Halafu hatutasikia mambo ya ndoto zake tena."

Reubeni, mwana mkubwa alikuwa na huruma kuliko wengine. Aliwambia, "Msimue, tumtupe katika hili shimo." Reubeni alipanga komwokoza Yusufu baadaye. Ndugu wengine walikubali.

Ndugu zake Yusufu walimtoa lile koti la rangi nyingi lizilo la kawaida. Wakamtupa ndani ya shimo mrefu. Halafu wakakaa chini kukula chakula chao. Reubeni akaondoka kwenda kuangalia kondoo.



Walipokuwa wakila chakula, waliona wafanya biashara fulani wakija na ngamia. Walikuwa wamebeba karafuu na vitu vingine vya dhamana kwenda kuuza kwa nchi ya Misri.

Yuda hakutaka kuacha Yusufu akufie ndani ya shimo. Aliona ni vyema wamuuze aende akuwe mtumwa. Nduguze walimtoa Yusufu kutoka kwa shimo. Walimuuza kwa vibande ishirini vya fedha. Yusufu alilia akiwasihi wasimuuze. Lakini hawakumsikiliza. Yusufu alichukuliwa na wafanya biashara. Yusufu alisafiri na kukaa karibu sana na nyumbani kwao Hebroni lakini alikuwa mtumwa hangeweza kutoroka.

Reubeni aliporudi na akapata Yusufu ameuzwa, aliudhika sana. Hao ndugu waliunda maneno watakayo ambia baba yao Yakobo. Waliuwa mwana mbuzi. Wakararua koti la Yusufu la rangi nyingi na kuchovya ndani ya damu. Walichukua hilo koti la damu na kumpelekea baba yao Yakobo. Walimdanganya kwamba wameipata njiani wakirudi nyumbani. Yakobo aliona kwamba Yusufu alikuwa ameuwawa na mnyama mkali. Aliona vibaya sana sana.

Yusufu alisafiri na wafanya biashara kwa siku nyingi. Hatimae walifika nchi ya Misri. Misri ilikuwa nchi kubwa ilitawaliwa na Farao. Wale wafanya biashara waliuza karafuu na vile vitu vyao vya dhamana. Waliuza Yusufu pia kama mtumwa. Matajiri wengi Misri walikuwa na watumwa. Potifa, akida mkuu wa askari wa Farao alinunua Yusufu. Alikuwa mtu wa maana kwa jeshi la Farao. Potifa alimchukua Yusufu nyumbani amfanyie kazi.

Yusufu alifanyia Potifa kazi kwa bidii. Potifa aliona kwamba Yusufu alikuwa mwaminifu na wakutegemewa. Potifa alimwamini Yusufu. Alimweka Yusufu asimamie kazi na utajiri wake wote. Yusufu alimwamini Mungu, ijapokuwa mtumwa kwa nchi ya mbali. Mungu alimlinda Yusufu. Alimpa bwana mzuri. Mungu alibariki nyumba ya Potifa kwa ajili ya Yusufu.